**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA AWALI NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**KIFURUSHI CHA LIKIZO APRILI- 2020**
**KISWAHILI V**

Muda; saa 1:30

**JINA: _______________________MKONDO_________ TAREHE: __________**

**MAELEKEZO**

- Mtihani huu una sehemu A,B,C na D
- Jibu maswali yote kwa umakini
- Usifutefute majibu
- Andika majina yako kwa herufi kubwa

**SEHEMU A: SARUFI**

1. "Tumalima" katika neno hili kiambishi cha nafsi ni kipi? ( )
   (a) -na- (d) -tu-
   (b) -ma- (e) Lima
   (c) -li-
2. Kauli taarifa ya sentensi isemayo, "Nataka Asha ajibu swali hili upesi" ni __________ ( )
   (a) Alitaka Asha ajibu swali lile upesi (c) Jibu swali lile upesi Asha alitaka
   (b) Asha alitaka ajibu swali lile upesi (d) Jibu swali Asha upesi alitaka
3. "Juma anacheza mpira uwanjani." Sentensi hii ikiwa katika hali ya mazoea itakuwa ipi kati ya hizi zifuatazo? ( )
   (a) Juma atacheza mpira uwanjani (c) Juma alicheza mpira uwanjani
   (b) Juma hucheza mpira uwanjani (d) Juma amecheza mpira uwanjani
4. Katika sentensi zifuatazo ipi ina maana sahihi
   (a) Sikuwa najua Edina ni dada yako (c) Sikuwa ninajua Edina ni dada yako
   (b) Sikuja kuwa Edina ni dada yako (d) Sikuwa ninajua kwamba Edina
5. Neno lipi kati ya haya yafuatayo ni kisawe cha neno "hifadhi"? ( )
   (a) Weka (c) Panga
   (b) Tunza (d) Ficha
6. Mtume! Haa! Yesu wangu! Loo! Ni maneno ya aina gani? ( )
   (a) Vitenzi (c) Viwakilishi
   (b) Vihisishi (d) Vivumishi
7. Ingawa walipata matatizo mengi safarini __________walifika salama. ( )
   (a) Hatimaye (c) Kwa hiyo
   (b) Kwa vile (d) Halikadhalika
8. Babu alikuwa analima shambani. Neno "alikuwa" ni aina ipi ya kitenzi? ( )
   (a) Kitenzi kikuu (c) Kitenzi kishirikishi
   (b) Kitenzi kitegemezi (d) Kitenzi kisaidizi
9. Watano wameshindwa kufika shuleni. Kiwakilishi katika sentensi hiyo ni kipi? ( )
   (a) Shuleni (c) Wameshindwa
   (b) Kufika (d) Watano
10. Vita ilipoanza nchini kongo watu wote_______ kitenzi kipi kinakamilisha sentensi hii? ( )
    (a) Walitweta (c) Walitaharuki
    (b) Walinusurika (d) Walitahamaki
11. "Mlicheza ngoma na kuimba usiku kucha" latola sentensi hii watenda ni nafsi ipi? ( )
    (a) Ya tatu wingi (c) Ya tatu umoja
    (b) Ya pili wingi (d) Ya kwanza wingi
12. Usikae hapa kwa kuwa ________maji mengi. ( )
    (a) Kuna (d) Pana
    (b) Ana (e) Muna
    (c) Mna

13. Hali ya kuona hay abaada ya kutenda au kufikiwa na jambo la feheha huitwaje? ( )
    (a) Tashwishwi (c) Woga
    (b) Tathimini (d) Tahayari
14. Uwoga wake umemponza. Neno "uwoga" ni aina ipi ya neno? ( )
    (a) Kielezi (d) Kivumishi
    (b) Kitenzi (e) Kiwakilishi
    (c) Nomino
15. Kinyume cha neno wao ni _______ ( )
    (a) Sote (d) Wale
    (b) Wowote (e) Sisi
    (c) Ninyi
16. Mpira uligonga mwamba nusura goli liingie. Neno lipi linaonesha kitenda? ( )
    (a) Nusura (d) Liingie
    (b) Mpira (e) Goli
    (c) Mwamba
17. Huyu ndiye kijana mwema. Katika sentensi hii kitenzi kishirikishi ni _______ ( )
    (a) Huyu (c) Mwema
    (b) Kijana (d) Ndiye
18. Ili tufaulu mitihani ______kusoma kwa bidi
    (a) Hatuna budi (c) Si budi
    (b) Tuna budi (d) Budi
19. "Wengi wamehamia shuleni kwetu" katika sentensi hiyo "wengi"limetumika kama aina gani ya neno? ( )
    (a) Kivumishi (d) Kitenzi
    (b) Kielezi (e) Kiunganishi
    (c) Kiwakilishi
20. Alimuita nyumani kwake kwa dhamira ya kumpa karo ya shule. Neno "dhamira"lina maana ipi? ( )
    (a) Dhamana (d) Dhamini
    (b) Madhumuni (e) Thumuni
    (c) Dhumuni

**SEHEMU B: LUGHA YA KIFASIHI**

21. Nahau isemayo, "Mtu mwenye ndimi mbili" ina maana ipi kati ya zifuatazo? ( )
    (a) Mropokaji (c) Kilimilimi
    (b) Mwongo (d) Kigeugeu
22. Wanafunzi walipotoka safari walilala usingizi wa pono. Msemo usemao, "usingizi wa pono" una maana gani? ( )
    (a) Usingizi wa mang'amung'amu (c) Usingizi mzito mno
    (b) Usingizi wa maruweruwe (d) Usingizi wa kustukastuka
23. Kitendawili kisemacho, " Kamba yangu ndefu lakini haiwezi kufunga kuni" kina maana ipi kati ya hizi zifuatazo? ( )
    (a) Mkufu (d) Treni
    (b) Nyoka (e) Njia
    (c) Waya
24. Methali isemayo "Mgaagaa na upwa hali wali mkavu" inatoa funzo gani? ( )
    (a) Bidi huleta mafanikio (c) Bidi huleta faraja
    (b) Mafanikio ni matokeo ya kazi (d) Bidi ni kazi ya kuhangaika
25. Usingelitia chumvi kwenye kile kikao wajumbe wasingeligombana. "kutia chumvi" ni usemi wenye maana gani? ( )
    (a) Kuongeza maneno yenye maudhi (d) Kuongeza maneno yasiyo na ukweli
    (b) Kuongeza maneno ya kustua
    (c) Kuongeza maneno ya utani

26. _________hufa maskini." Kifungu kipi hukamilisha methali hiy kw ausahihi?
   (a) Anayeiba cha nduguye
   (b) Anayekula cha nguguye
   (c) Mtegemea cha nguguye
   (d) Mkimbilia cha nduguye
   ( )

27. "Mchelea mwana kulia hulia yeye mwenyewe" methali hii inatoa funzo gani?
   (a) Mtoto asipofunzwa vema huaibisha
   (b) Bora kulea kuliko kulelewa
   (c) Kuhofia kulea si malezi bora
   (d) Malezi yam toto husababisha hofu
   ( )

28. "Heri kufa macho kuliko ________". Methali hii hukamilishwa na kifungu kipi cha maneno?
   (a) Kujikwaa ulimi
   (b) Kuumia moyo
   (c) Kuzama majini
   (d) Kufa moyo
   ( )

29. Chagua methali ambayo ni kisawe cha chovyo chovyo humaliza buy la asili
   (a) Kidogo kidogo hujaza kibaba
   (b) Bandu bandu huisha gogo
   (c) Akiba haiozi
   (d) Maji yakimwagika hayazoleki
   ( )

30. Hana miguu lakini huenda mbio sana. Tegua kitendawili hiki.
   (a) Mchawi
   (b) Shetani
   (c) Upepo
   (d) Mbwa

**SEHEMU C: UFAHAMU**

Soma habari ifuatayo kwa makini kisha jibu maswli yaliyoulizwa

Mlima Kilimanjaro upo hapa kwetu Tanzania. Ni mlima mrefu Zaidi hapa nchini na barani Afrika. Mlima huu umefunikwa na theluji kileleni. Theluji nyeupe huu fany amlima ung'ae sana. Katika miaka ya karibun theluji imepungua sana. Kutokana na ongezeko la joto duniani. Hali ya ongezeko la joto imesababishwa na uharibifu wa mazingira. Watu huchoma moto misitu na hifadhi za Wanyama zilizoko jirani. Hali ya joto husababisha theluji kuyeyuka kidogokidogo hivyo kuzidi kupungua mwaka hadi mwaka.

Watalii kutoka nchi za mbali huja Tanzania kuona mlima huo unaovutia. Baadhi yao huupanda hadi kileleni. Nchi yetu hunufaika na kuja kwao kwa sababu hulipa fadha za kigeni serikalini kwa huduma mbalimbali wanazopata. Pia vijana wetu hupata ajira ya kuwaongoza hapa na pale wanakotaka kwenda. Wauza vyakula na wafanya biashara wengine hupata pia soko la bidha zao.

Maswali:

31. Zifuatazo ni sifa za mlima kulimanjaro isipokuwa:-
   (a)
   (b) Una theluji
   (c) Ni mrefu sana
   (d) Huvutia watalii
   (e) Uko kusini mwa Tanzania
   ( )

32. Nchi yetu hupata faida gani kutokana na mlima huo?
   (a) Watalii wengi
   (b) Huingiza fedha za kigeni
   (c) Vyakula huuzwa
   (d) Una Wanyama wakali
   ( )

33. Wageni kutoka ng'ambo wanaokuja kuupanda mlima Kilimanjaro huitwaje?
   (a) Wazungu
   (b) Raia wa kigeni
   (c) Wasio waatanzania
   (d) Watalii
   ( )

34. Kuongezeka kwa joto duniani kumeathirije mlima huo?
   (a) Kupungua watalii
   (b) Kumeyeyusha theluji
   (c) Mlima hulipuka lipuka
   (d) Kuzuka kwa moto
   ( )

35. Watalii wengine huupanda mlima huo hadi kileleni. Neno kileleni lina maana gani?
   (a) Sehemu ya juu kabisa
   (b) Pembezoni
   (c) Mwanzoni
   (d) Katikati
   ( )

**Andika kauli halisi zifuatazo kuwa kauli taarifa**

36. “Mchote  maji muoge” baba aliwaambia
    - ✓ ________________________________________________

37. “Ulimwona Edina?” Leania alimuuliza Baraka
    - ✓ ___________________________________________________

38. “Msicheze barabarani. “ Dada alituambia
    - ✓ ______________________________________________________

Badili kauli taarifa kuwa kauli halisi

39. Mwalimu alimuuliza Linah kama alifanya kazi  ya nyumbani
    - ______________________________________________________________________

40. Shangazi aliniambia kuwa niende kumtembelea nyumbani kwake siku ya jumapili
    - _________________________________________________________________________

**SEHEMU D: UTUNGAJI**
Panga vipengele vya barua ya kirafiki vifuatavyo katika mtiririko unaofaa uonyeshe mpangilio sahihi wa barua ya aina hiyo kwa kuweka herufi A-E

41. Barua yenyewe (madhumuni) (     )
42. Salaamu (     )
43. Mwisho wa barua (     )
44. Tarehe (     )
45. Anuani ya mwandishi (     )